# TARGETER WINGS

## KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

Wings 004

# GREDI 5 - 2021

# SHUGHULI ZA KISWAHILI

**Jina** ..........................................................................................................................................

**Jina la shule** ..........................................................................................................................

**Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.**

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Viwango vya kutathmini | | | | | | | | |
| | Kuzidisha matarajio | | Kufikia matarajio | | Kukaribia matarajio | | Mbali na matarajio | |
| Kusikiliza na Kuzungumza | 5 | | 4 | | 3 | | 0 - 2 | |
| Kusoma kwa sauti | 91 na zaidi | | 61 - 90 | | 31 - 60 | | 0 - 30 | |
| Sarufi | 19 - 20 | | 10 - 18 | | 6 - 9 | | 0 - 5 | |
| Ufahamu | 5 | | 4 | | 3 | | 0 - 2 | |

## SEHEMU YA KWANZA

**I. Kusikiliza na kuzungumza (Alama 5)**

**Mwalimu amwamkue mwanafunzi kisha ajitambulishe.**

Mimi ni mwalimu ________________ na ningependa tuongee kuhusu heshima na adabu.

a) Jibu la shikamoo ni gani? ***(Mwanafunzi ajibu)***

b) Rafiki yako akiumia wakati mnacheza, utamwambiaje? ***(Mwanafunzi ajibu)***

c) Ukipewa zawadi na mwalimu utamwambiaje kumshukuru? ***(Mwanafunzi ajibu)***

d) Huwa unatumia neno gani la heshima kumrejelea mwalimu wako wa kiume? ***(Mwanafunzi ajibu)***

e) Elezea jinsi utamwomba mwalimu wako ruhusu ukitaka kuenda haja. ***(Mwanafunzi ajibu)***

## II. KUSOMA KWA SAUTI

**Soma kifungu kifuatacho kwa sauti mwalimu akisikiliza.**

Moto huweza kuanzishwa kwa njia nyingi. Wakati mwingi hutumika kupika chakula na kuwapa watu joto wakati wa baridi. Moto huwa na faida nyingi lakini pia husababisha madhara.

Moto huweza kutokea kama ajali na kuua, kuteketeza vitu vya gharama kubwa, majumba, misitu na kuyaharibu mazingira. Kwenye majumba moto huweza kuanzishwa na hitilafu wa umeme au gesi, stovu na matumizi mabaya ya mafuta taa, petroli au makaa.

Iwapo moto utatokea popote, jaribu kuuzima mara moja. Ukiona kuwa umezidi, piga kelele kuomba msaada huku ukijiepusha na hatari. Kama kuna simu wapigie wazimamoto wafike mahali hapo haraka. Kama kuna vifaa vya kuzima moto, vitumie. Jaribu kuondoa vitu ambavyo ni muhimu na hasa vile vinavyoweza kueneza moto.

## III. UFAHAMU (Alama 10)

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Wanyama wa nyumbani, au mifugo ni wale wanyama ambao huishi katika mazingira ambayo mwanadamu anaishi na hawawezi kumuathiri kwa kiasi kikubwa. Wanyama hao wanatunzwa kwa uangalizi wa binadamu kwa ajili ya ulinzi, michezo, pambo na chakula.

Mmoja wa wanyama wafugwao ni ng'ombe. Ng'ombe ni mnyama ambaye ana pembe, miguu minne na nundu. Mnyama wa porini ambaye hufanana na ng'ombe ni nyati. Kunao ng'ombe ambao hawana pembe wala nundu. Ng'ombe wa kiume ambaye amekomaa huitwa fahali, naye wa kike huitwa mbuguma.

Ng'ombe ana **faida** nyingi sana katika maisha yetu. Jambo la kwanza, ng'ombe hutupa chakula. Chakula ambacho hutokana na ng'ombe ni nyama na maziwa. Nyama huweza kuliwa pamoja na ugali, wali au chapati. Maziwa nayo huweza kutumika kupikia chai, uji au kuongezwa katika mboga au kunywewa moja kwa moja. Nyama na maziwa hujenga mwili wa yule anayetumia. Mifupa na nyama ya ng'ombe huweza kutokoswa na kuunda mchuzi ambao huongeza nguvu kwenye mifupa.

1. Wanyama wa nyumbani pia huitwa ______________________

2. Taja jina jingine la mnyama 'nyati'. ______________________

3. Eleza maana ya fahali kulingana na ufahamu.

______________________________________________

4. Kinyume cha neno faida ni ______________________

5. Ng'ombe ni mmoja wa wanyama wanaofugwa. Taja wanyama wengine wawili wa nyumbani. ______________ ______________

6. Taja vyakula viwili ambavyo huliwa pamoja na nyama kulingana na ufahamu.

______________ ______________

7. Nyama na maziwa huleta faida gani mwilini?

______________________________________________

8. Mifupa na nyama ya ng'ombe ikitokoswa huunda nini?

______________________________________________

## IV. SARUFI (Alama 20).

**Tambua nomino za pekee kwenye sentensi zifuatazo.**

1. Amina ameenda sokoni kununua mboga.

______________________________________________


2. Tutaenda jijini Nairobi mwaka ujao.

______________________________________________


3. Mto Tana hufurika wakati wa msimu wa masika.

______________________________________________

**Andika majina ya maumbo haya.**

4. 

______________________

5. 

______________________

**Kanusha sentensi zifuatazo.**

6. Maziwa ya mama yamwemwagika.______________________________

7. Jua litawaka sana. ______________________________

8. Maua yale yanafanana na nyota. ______________________________

**Akifisha sentensi zifuatazo.**

9. je unajua kuendesha gari ______________________________

10. baba ameenda nchini tanzania ______________________________

**Andika majina ya vyombo hivi.**

11. 

____________________

12. 

____________________

**Kamilisha methali:**

13. Mgema akisifiwa ______________________________

14. Mvumilivu hula ______________________________

**Andika sentensi zifuatazo kwa wingi:**

15. Ukuta uliopakwa rangi nyeupe unapendeza

________________________________________

16. Mti mkubwa ulikatwa na mwanafunzi.

________________________________________

***Tegua vitendawili hivi:***

17. Ajenga ingawa hana mikono ______________________________

18. Adui lakini popote uendako yuko nawe ______________________________

***Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao.***

19. Mama anapika chakula kitamu

________________________________________

20. Mwalimu wetu anasoma kitabu cha hadithi.

________________________________________